

**HOTUBA YA MHE. ANNA E. MGHWIRA, MKUU WA
MKOA WA KILIMANJARO KWENYE MAPOKEZI YA
WAPANDA MLIMA NA WAENDESHA BAISKELI WA
KAMPENI YA "*KILIMANJARO HIV AND AIDS
CHALLENGE*" TAREHE 09, JUNI, 2017 -
LANGO LA MWEKA**

- **Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro;**
- **Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Rombo;**
- **Mhe. Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya Moshi;**
- **Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS);**
- **Mkurugenzi Mtendaji Geita Gold Mine;**
- **Viongozi wote wa Serikali na viongozi wa Vyama vya Siasa;**
- **Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA);**
- **Washiriki wa '*Kilimanjaro HIV & AIDS challenge 2017*;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana:**

Ninayo furaha kubwa sana kualikwa kuwa mgeni rasmi katika tukio hili kubwa la kuwapokea mashujaa wetu waliopanda na waliozunguka Mlima Kilimanjaro mwaka 2017 kwa lengo la kuchangisha fedha za mwitikio wa VVU na UKIMWI - **Asanteni Sana!**

Leo tunashuhudia na kuwapokea waliopanda Mlima (*Climbers*) na waliozunguka Mlima (*Cyclists*), hakika hawa ni mashujaa wa kuigwa na wanastahili pongezi za kipekee kwa mchango wao katika kuhakikisha kwamba Kampeni hii inafanikiwa – **HONGERENI SANA!**

Ndg. Wapanda Mlima, Waendesha Baiskeli na Wageni Waalikwa;

Uzinduzi wa Kampeni ya *Kilimanjaro HIV and AIDS Challenge 2017* ulifanyika Jijini Dar es Salaam, mwezi Aprili, 2017 ambapo Makamu wa Rais Mstaafu, Dk. Mohamed Gharib Bilal, alifanya uzinduzi huo. Leo kwa pamoja, tunashiriki hitimisho la kampeni hii ya mwaka **2017** tunapo wapokea mashujaa wetu waliopanda na kuzunguka Mlima Kilimanjaro.

Tunawapongeza wapanda mlima **50** na waendesha baiskeli **37** kwa mafanikio mliofikia, mafanikio yenu yanadhihirisha kuwa; mwitikio dhidi ya **VVU** na **UKIMWI** unawezekana iwapo tutashirikiana.

Ndg. Wapanda Mlima, Waendesha Baiskeli na Wageni Waalikwa;

Sote tunatambua kwamba Kampeni hii ina malengo kadhaa, yakiwepo:-

- Kutoa fursa na hamasa kwa wadau kujadili maswala ya VVU na UKIMWI;
- Kutafuta rasilimali fedha na kutoa kwa wadau wanao tekeleza shughuli za mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini;
- Kuwapatia fursa wapanda mlima wa ndani ya nchi pamoja na Mataifa mbalimbali kupanda Mlima Kilimanjaro ambao ni mlima mrefu Afrika. Aidha, kwa namna ya pekee kwa mara ya pili mwaka huu tumeshuhudia ushiriki wa waendesha baiskeli kwenye kampeni hii;

- Kujenga umoja wa Kitaifa katika mwitikio dhidi ya VVU na UKIMWI, hususani ushirikiano kati ya sekta ya Umma na Binafsi - Public Private Partnership (PPP),
- Kuongeza uelewa wa maswala ya VVU na UKIMWI nchini, na
- Mwisho, ni kuoanisha changamoto za VVU na UKIMWI zilizo tambuliwa na serikali, na mipango iliyoanishwa ya utekelezaji.

Ndg. Wapanda Mlima, Waendesha Baiskeli na Wageni Waalikwa;

Ni dhahiri kwamba Kampeni hii ina mchango mkubwa katika kufikia kampeni ya kitaifa ya **SIFURI TATU - *Kutokuwa na Maambukizi Mapya, Kutokuwa na Unyanyapaa na Ubaguzi, na Kutokuwa na Vifo Vitokanavyo na UKIMWI.***

Aidha, napenda kuzihamasisha jumuiya za wafanyabiashara, makampuni na sekta binafsi pamoja na watanzania kwa ujumla, kuunga mkono Kampeni ya **"Kili Challenge"** kwa miaka ijayo na kujitokeza kwa wingi kushiriki na kufadhili

washiriki wa kampeni, kwa lengo la kupata fedha za kutosha kufikia malengo ya Kitaifa ya mwitikio wa **VVU** na **UKIMWI**.

Mwisho; kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Mgodhi wa Dhahabu wa Geita (GGM) kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) pamoja na wadau washiriki, katika kuandaa na kuwezesha Kampeni ya **"Kilimanjaro HIV and AIDS Challenge"** kila mwaka. Vile vile, natambua jitihada zinazofanywa na Sekretariet ya Mkoa na Wilaya za Hai na Moshi kwa kuratibu na kuwa wenyeji wa tukio hili kila mwaka. **Asanteni Sana!**

Ndg. Wapanda Mlima, Waendesha Baiskeli na Wageni Waalikwa;

Baada ya maelezo hayo; napenda kutangaza kwamba **"Kilimanjaro HIV and AIDS Challenge 2017"** imehitimishwa rasmi.

Ahsante Sana!